**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA WAZIRI MKUU**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

# MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI KATENTE

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS – TAMISEMI**
**SHULE YA SEKONDARI KATENTE**

**Mkuu wa Shule 0759198069**
**Makamu Mkuu wa Shule 0755284833**
**Matron/Patron 0752810104/075601915**
**Shule ya Sekondari Katente,**
**S.L.P 67,**
**BUKOMBE.**
**Tarehe ........................…**

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ………….............................................................**
**S.L.P ……………………………………..**
**BUKOMBE.**

Yah**: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI KATENTE ILIYOKO HALMASHAURI YA BUKOMBE MKOA GEITA MWAKA .............**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka 2026 na atasoma tahasusi ya ….……… Shule ya Sekondari Katente ipo umbali wa Kilometa 1.5 Magharibi mwa makao makuu ya Halmashauri ya wilaya ya Bukombe. Unapofika katika kituo cha mabasi Ushirombo Nauli ni Shilingi 2,000/= kwa pikipiki na Shilingi 3000 kwa bajaji.

Muhula wa Masomo unaanza tarehe ................ hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe .............. Mwisho wa kuripoti ni tarehe .................

2.0 **Mambo muhimu ya kuzingatia:-**

2.1 **Sare za Shule**

i. Sare ya shule hii ni sketi 2 za rangi ya **ugoro iliyokoza** zenye malinda ya box kitambaa kiwe kizito cha suti na **sketi iwe ndefu inayofika kwenye FUNDO ZA MIGUU kwa Wasichana**

ii. Suruali 2 za rangi ya **ugoro iliyokoza** zenye malinda mawili, ndefu **INAYOFUNIKA VIATU** na kwa chini iwe na mkunjo (turn up) na **zisiwe modo (upana chini iwe nchi16)** kwa Wavulana. Angalia kiambatanisho cha mchoro wa picha **‘C’**

iii. Shati 2 nyeupe za mikono mirefu zisiwe za kitambaa cha **HARUWA** (Chenye ubleu).

iv. Rangi ya Hijab (juba) ni nyeupe isiwe ya kitambaa cha **HARUWA** (Chenye ubleu) ifunike kifua cha mwanafunzi pia iwe ndefu kufikia vifundo vya mikono akisimama .
v. Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi.
vi. Soksi jozi mbili nyeupe.
vii. Mkanda mweusi wa ngozi wa kuvalia suruali kwa wavulana.
viii. Sweta rangi ya **kijivu.**
ix. Sketi nyeusi 1 **yenye marinda 16 kitambaa kiwe kizito cha suit** na iwe ndefu **inayofika kwenye FUNDO ZA MIGUU kwa wasichana**.
x. Suruali 1 ya **rangi nyeusi** yenye malinda mawili, ndefu **INAYOFUNIKA VIATU** na kwa chini iwe na mkunjo (turn up) na **isiwe modo (upana chini iwe nchi16)** kwa Wavulana. Angalia kiambatanisho cha mchoro wa picha **'C'**
xi. Tai ndefu rangi ya ugoro iliyokoza.
xii. Tisheti (T-shirt) yenye kora, rangi ya blue bahari (light blue) **iliyokoza** yenye nembo ya shule **zinapatikana shuleni kwa Tsh.12000/=**

**b. Sare ya Michezo ni**

**1.** Jezi ya blue na Raba
**2.** Full Truck suit ya blue Kwa wasichana na wavulana
**3.** Sketi fupi ya bluu ya solo(tetroni) yenye riboni nyeupe chini isiyovuka magoti itakayovaliwa juu ya Trakisuti ya michezo kwa waschana.

**NB: Truck suit isiwe fupi wala ya kubana**

2.2 **Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-**

i. Madaftari Counter books 7 za 4Quire au 3Quire
ii. **Ream (A4)** Double **'A'** Mbili (2) kwa mwaka wa masomo.
iii. Flat file folder kwa ajili ya kutunza kumbukumbu zako.
iv. 0xford Advanced Learners Dictionary kwa matumizi yako na kamusi ya Kiswahili
*v.* Vitabu vya masomo ya tahasusi husika, kwa hapa tuna **HGK, HGL** na **HGLi.** Nunua vitabu vya **TIE** mtaala mpya pia kwa **HISTORY** ongeza **1.** *History Book 1 by Idrisa Ramadhan Msuya* **2**. *Basic facts about world history new syllabus by Shibitali Tumaini*
vi. Scientific Calculator kwa wanafunzi wanaosoma Jiografia.
vii. Kwanja 1, jembe 1, mfagio 1 wa nje (chelewa)
viii. Hati maalumu ya vipimo vya daktari kuthibitisha hali ya Afya yako (fomu imeambatishwa)

2.3 **Michango mbalimbali**

| **Na** | **Aina ya Mchango** | **Kiasi** |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 35,000/= |
| 2. | Tahadhari | 5,000/= |
| 3. | Nembo | 5,000/= |
| 4. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

**Michango hii ilipwe kwenye Account ya Shule.**

**NMB ACCOUNT NO :32501200048**

**JINA LA AKAUNT: KATENTE SEKONADARI**

**Kila Mwanafunzi aje na KADI YA BIMA ya Afya kwa ajili ya Matibabu. Kama hana aje na shilingi 50,400/= kwa ajili gharama za BIMA YA AFYA kwa mwaka.**

## 3.0 Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule.
iii. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
iv. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
v. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vi. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
vii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
viii. Kutunza mali za shule;
ix. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
x. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi**
- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

### 3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni.
vii. Kufuga ndevu**;**
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xii. Kusababisha mimba;
xiii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiv. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xvi. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xviii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**Viambatisho na Fomu Muhimu**

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;
iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na
iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- **Mkuu wa shule 0759198069/0621941441**
- **Makamu Mkuu wa Shule 0755284833/0621256704**
- **Mwandamizi Taaluma 0755496193**
- **Mwandamizi Malezi 0628410910**

**KARIBU SANA KATENTE SEKONDARI**

**………………………**
**SAYI . M. GIBE**

**MKUU WA SHULE**

# KIAMBATANISHO "A"
# SHULE YA SEKONDARI KATENTE S.L.P 67, BUKOMBE

## 1. MAELEKEZO BINAFSI KUHUSU HISTORIA YA MWANAFUNZI

**(Ijazwa na mzazi/mlezi au mwanafunzi kabla ya kuja kuripoti shuleni)**

(i) Jina la mwanafunzi ……………………………………………………Tarehe ya kuzaliwa ……………………….

(ii) Shule ya sekondari aliyotoka…………………………………………………………..……………………………..

(iii) Jina la Baba/Mlezi………………………………………………………… kazi yake ……………………………….

(iv) Jina la Mama/Mlezi……………………………………………………….. kazi yake………………………………..

(v) Kijiji/kitongoji/mtaa wazazi/walezi wanakoishi …………………………. wilaya………………… mkoa………....

(vi) Jina la mwenyekiti wa kitongoji …………………………………………… No ya simu…………………………

(vii) Dini ya mwanafunzi……………………………………………………………………………………………………..

(viii) Majina ya ndugu wa karibu na mwanafunzi wanaoweza kutoa msaada pindi wakihitajika (hawa ni ndugu wengine tofauti na wazazi/walezi ambao wanaweza kufika kumsalimia au kumletae mahitaji au mzazi/mlezi anapokuwa hayupo wanaweza kuwa wawakilishi wake **(NI MUHIMU WAJULIKANE KWANI AKIJA TOFAUTI NA HAPO HATAPATA HUDUMA).**

(a) Jina ………………………………………………………………… anakoishi ……………………….. simu ……….....……

(b) Jina ………………………………………………………………… anakoishi ………………………simu……..…..……

(c) Jina ………………………………………………………………… anakoishi ………………………simu………..…..

(d) Jina ………………………………………………………………… anakoishi ………………………simu……….…..

NB. Je wazazi wako wapo wote hai ………………… (ndiyo/hapana) kama amefariki/wamefariki aliyefariki ni …………… (mama/baba) kama wewe ni yatima mlezi wako wa karibu ni …………………………………………..

## 2. FOMU YA MKATABA KUKUBALI SHERIA NA TARATIBU ZA SHULE.

Mimi (jina la mwanafunzi) …………………………………. Naahidi sitashiriki kabisa katika migomo/fujo/utoro wa kujificha na kutenda makosa ya jinai shuleni na maeneo mengine. Pia ninaahidi kuzifuata sheria na taratibu za shule kikamilifu kwa faida yangu binafsi, shule na Taifa kwa ujumla.

Endapo nitakwenda/nitafanya kinyume na taratibu na kanuni za shule nakubali kufukuzwa shule, ama kusimamishwa masoma ama kufikishwa mahakamani na kupewa adhabu yoyote kwa mujibu wa sheria.

Jina la mwanafunzi…………………………………………………………………………… sahihi ………………………..

Jina la mzazi/mlezi…………………………………………………………………………… sahihi………………………….

Jina la kiongozi wa mtaa…………………………………………………………………….. sahihi…………………………

## FOMU YA MZAZI/MLEZI KUKUBALIANA NA SHERIA NA KUTEKELEZA MAELEKEZO YA SHULE.

Mimi mzazi/mlezi wa ………………………………………………….. nakili kukubaliana na sheria, kanununi na kutekeleza maelekezo yatakayotolewa na uongozi wa shule/Bodi ya shule.

Aidha, naahidi kutoa ushirikiano wa hali ya juu kwa uongozi wa shule pindi nikihitajika kuhusu tabia, mwenendo au suala jingine lolote linalomuhusu mtoto wangu.

Jina la mzazi/mlezi ……………………………………………………………………….. sahihi ……………………………

Jina la mwenyekiti wa kitongoji …………………………………………….……sahihi ……………………………………

**KIAMBATANISHO ‘B’**
**KATENTE SECONDARY SCHOOL**
**P.O.BOX 67, BUKOMBE**
**STUDENT MEDICAL EXAMINATION FORM**

To the medical officer.
……………………………………..
……………………………………

**PERSONAL HISTORY**

First Name ………………………………………….. other Name ……………………age …….. Gender……..

Please Examine the above as to his/her fitness for under going the studies. Date ………………………………

(a) Respiratory diseases ……………………………………………Tuberculos is…………………………..
(b) Cardiac diseases …………………………………………………………………………………………….
(c) Gastro – intestinal diseases ……………………………………………………………………………..
(d) Renal or genital urinary diseases ……………………………………………………………………….
(e) Syphilis or gonorrhea ……………………………………………………………………………………
(f) Emotional disease or Psychosis …………………………………………………………………………
(g) A history of serious injuries ……………………………………………………………………………..

**PHYSICAL EXAMINATION**

(1) Height ……………………………………. (2) weight …………………….. (3) Chest – lungs ……………………………
heart ………………………………. BP……………………………………….. (4) abdomen any organs ……………………………………. other mass ……………………………… Pregnancy (girls)(5) Skin disease ……………………...... (6) Eye conjunctive …………………………… Sight: without glasses ………………………..
Sight: with glasses ………………………….
(7) ENT: ……………………………………………………………………………………………………

**LAB INVESTIGATION**


(a) ESR ……………………………….. (b) WBC…………………….. (c) Bs/mps………………
(d) MRDT………………………….. (e) Stool ……………………. (f) URINE……………………..
(8) Any physical challenges of the prospective student plus the Doctor’s recommendations.
………………………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………

**CONCLUSION**

I have examined …………………………………. and considered that he/she is fit/not fit to be enrolled as a student at KATENTE SECONDARY SCHOOL.

Name ……………………………………………………………………. Signature …………………
Title ……………………………………………………………………
Qualitifications …………………………………………………………… (Official stamp)
Date ……………………………………………………………………




KIAMBATANISHO "C"
MBELE
NYUMA
MBELE
Inchi 2
NYUMA
Inchi 2
SARE YA SHULE INAYOKUBALIKA